**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIAOFISI YA RAIS TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**

**Kumb. Na. VSS/VOL.17/JOINING/2021**

SHULE YA SEKONDARI VUMARI
S.L.P 60
**SAME**
10/12/2020

**YAH: MAAGIZO KWA MZAZI WA MWANAFUNZI ANAYEJIUNGA NA SHULE YA SEKONDARI VUMARI MWAKA 2021.**

Nafurahi kukujulisha kuwa mwanao……………………………………………………..……mwenye namba ya mtihani ………………………………………………. amechaguliwa kujiunga na kidato cha kwanza katika shule hii. Mwanafunzi anahitaji kuripoti shuleni siku ya kufungua shule bila kukosa tarehe 11/01/2021 saa 1:00 Asubuhi.

**SHULE ILIPO.**
Shule ya Sekondari Vumari ipo katika Kijiji cha Vumari, Kata ya Vumari kilometa 6 Mashariki mwa kijiji cha Ishinde kilichopo barabara ya Moshi - Dar es Salaam km10 kutoka mjini Same.

**MAHITAJI YA SHULE.**

1. **MALIPO NA MICHANGO YA SHULE**.
   a) Mchango wa chakula cha mchana kwa mwaka ni **Tshs. 100,000**/= au **Tshs. 50,000**/= kwa mhula. _Kila mwanafunzi akiripoti shuleni aje na malipo ya chakula ya mhula wa kwanza ambayo ni **Tshs. 50,000** tu ili aweze kushiriki mlo wa mchana.

2. **SARE YA SHULE**
   **a) WAVULANA**
   - Mashati mawili (2) meupe aina ya Tetron mikono mifupi mapya (yasiwe mitumba).
   - Suruali jozi mbili rangi ya **daki bluu** na nzito zenye marinda na mifuko mitatu miwili ya mbele na mmoja nyuma wa kuchimbia na sio modo.
   - Viatu vipya rangi nyeusi vya kamba.
   - Soksi ndefu rangi nyeusi jozi mbili
   - Raba jozi mbili kwa ajili ya michezo
   - Bukta rangi ya blue ya michezo.

   **b) WASICHANA**
   - Blauzi mbili (2) nyeupe tetroni mikono mifupi mapya
   - Viatu vya ngozi nyeusi visivyo na visigino virefu jozi mbili (vya kamba).
   - Soksi ndefu nyeupe jozi mbili.
   - Raba jozi mbili kwa ajili ya michezo

- Nguo za michezo pamoja na bukta yake rangi ya bluu
- Sketi jozi mbili rangi ya **daki bluu** (mshono uwe rinda box).

c) **NGUO ZA KUZUIA BARIDI**:
Kila mwanafunzi anatakiwa kuwa na sweta ya mshono wa V shingoni rangi ya **daki bluu**

3. **CHAKULA CHA MCHANA**:-
Wazazi wanachangia chakula cha mchana na uji wa saa nne asubuhi. Kama ilivyoainishwa hapo juu kwenye orodha ya mchango wa chakula kwa wanafunzi. Kila mwanafunzi anatakiwa kuwa na vyombo vya chakula kama sahani, kikombe na kijiko, vyombo viwe vya rangi husika. Mzazi jitahidi kumlipia mwanao chakula cha mchana ili awe na afya njema kimwili na kiakili.

4. **VIFAA VYA TAALUMA**
Tafadhali mwandae mwanao kikamilifu kwa kumpatia vifaa muhimu vya kukuza taaluma yake awapo shuleni.

Vifaa hivyo ni:-
- Daftari kubwa kumi na moja (11) counter Books).
- Kamusi ya Kiingereza (English to English Dictionary)
- Mathematical seti 1
- Rula 1
- Penseli ya HB na kalamu ya bluu au nyeusi
- Mfuko (begi) la kubebea vitabu
- Fail kwa ajili ya kutunzia mitihani

5. **VIFAA VYA UZALISHAJI MALI NA USAFI WA MAZINGIRA**

**I).WAVULANA**
- Panga jipya 1 na slesha 1
- Ndoo ndogo yenye ujazo wa lita 10
- Ufagio mgumu (chelewa).

**II) WASICHANA**
- Aje na jembe jipya na mpini wake na squeezer
- Ndoo ndogo yenye ujazo wa lita 10
- Ufagio mgumu (chelewa).

6. **SHERIA ZA SHULE**

Pamoja na barua hii naambatanisha nakala ya sheria za shule. Tafadhali mkabidhi mwanao sheria za shule azisome na kuzielewa vizuri na kuzifuata. Msisitize mwanao afuate sheria za shule kikamilifu.

**7. AFYA YA MWANAFUNZI**

Tafadhali mpeleke mwanao akapimwe na Daktari wa Hospitali ya Serikali au Kituo cha afya cha Serikali na kujaziwa fomu ambayo tumeambatanisha. Fomu hii irudishwe shuleni anaporipoti mwanafunzi.

**8. MASOMO**

Masomo yataanza rasmi tarehe 11/01/2021 asubuhi. Hakikisha kuwa mwanao anakuwepo. Aidha unashauriwa kumhimiza mwanao kuhudhuria na kuwahi shuleni ili kuborehsa taaluma yake.

Nakukaribisha sana kwenye jumuiya ya shule na namkaribisha sana mwanao kwenye Elimu ya Sekondari.

**9. MTIHANI**

Kutakuwa na mtihani wa kuwapima wanafunzi watakaoingia kidato cha kwanza mwaka 2021 tarehe 18/01/2021. Msisitize mwanao kuwahi siku ya kufungua shule.

**KARIBU SANA!**

Wako katika Elimu,

**………………**

**MKUU WA SHULE.**

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**SHULE YA SEKONDARI VUMARI- SAME.**

**SHERIA ZA SHULE**

Jumuiya ya shule ya Sekondari Vumari ni kitu kimoja na tunafikiri na kuwaza pamoja yale ambayo yatailetea jamii yetu maendeleo ya kweli na kufanya Vumari kuwa mahali pa kupendeza na kutamanika kuishi. Moto wetu ni ***ELIMU NI NGUZO (EDUCATION IS POWER).***

**SHERIA ZA SHULE**

**A: HESHIMA**.

1. **Heshima kati ya mwanafunzi**

Moto wa shule ni kuona kwamba

a) Wanafunzi wanapenda na kuheshimiana
b) Wataheshimu viongozi waliowachagua
c) Wanafunzi wanashirikiana na kusaidiana nje na ndani ya madarasa
d) Matumizi ya lugha chafu, matusi, matukano masengenyo pia kupigana ni marufuku popote pale mwanafunzi anapokuwa nje au ndani ya darasa.

2. **Heshima kwa Walimu na Wafanyakazi wasio walimu**

a) Wanafunzi wanalazimika kusimama anapopita mwalimu. Mfanyakazi mwingine,pamoja na watu waliowazidi umri. Wanafunzi wanapaswa kusalimua kwa heshima wale wote waliowazidi umri au madaraka.
b) Wanafunzi wanapaswa kuelewa kuwa walimu na wafanyakazi wa shule ni walezi wao. Hivyo ni lazima kuwaheshimu bila ubaguzi.
c) Utani wowote ule kati ya walimu/wafanyakazi wa shule na wanafunzi ni marufuku.

3. **Heshima kwa jumuiya nje ya shule**

a) Wanafunzi wanalazimika kuwaheshimu viongozi wote wa umma kwa ujumla. Watatakiwa kujiweka tayari wakati wowote kujitolea kwa shughuli mbalimbali za ujenzi wa Taifa inapolazimika.
b) Wageni wote wanapofika shuleni wanapokelewa kwa heshima na kupewa msaada wa kupelekwa kwa mwalimu wa zamu ambaye ataelewa ni wapi pa kumpeleka.

4. Heshima katika kazi uvivu, uzembe na utegaji katika kazi zingine uwe ni mwiko kwa kila mwanafunzi.

5. **Heshima katika mali**

a) Kila mwanafunzi anatakiwa kuwa mwaminifu katika mali yake na wanafunzi wenzake.

b) Utunzaji wa mali ya umma unapewa kipaumbele na ni sharti kila mwanafunzi kutumia vifaa vyote vya shule kwa uangalifu mkubwa. Uharibifu wa kifaa chochote cha shule ni lazima uripotiwe kwa mwalimu wa zamu bila kuchelewa.
c) Uharibifu upotevu na uvunjaji wa mali ya shule ni lazima aliyehusika kulipa kama mali ya shule imeharibiwa au kupotezwa na kikundi bila kumtaja aliyehusika basi kikundi chote kitawajibika kulipa mali hiyo.
d) Ni marufuku kuandika katika vitabu vya shule, madawati na viti pia ukutani.

6. **HESHIMA KWA TAIFA**.

Wanafunzi wanawajibika kuonyesha heshima ya juu na kuwa na nidhamu ya dhati kwa:-

i) Bendera ya Taifa (National Flag).
ii) Nembo ya Taifa
iii) Wimbo wa Taifa
iv) Fedha za Taifa
v) Picha za viongozi wa serikali
vi) Viongozi wa serikali.

**B. USAFI**.

a)Kila mwanafunzi lazima awe msafi wa mwili ,akili na mawazo.Sare ya shule ni lazima iwe safi nyakati zote na iwe inaonyesha heshima.

❖ **WASICHANA.**

Nywele zikatwe na kuchanwa (Hairuhusiwi kunyoa mitindo ya kihuni).Ni marufuku kuvaa herein,pete,wigi,bangili,kupaka wanja,kupaka hina na manukato mengine.Pia hairuhusiwi kwa mwanafunzi kufuga kucha ndefu na kupaka rangi.

❖ **WAVULANA.**

Nywele zikatwe na kuchanwa (Huruhusiwi kunyoa mitindo ya kihuni na kufuga ndevu)

**USAFI WA TABIA**.

1.Ni marufuku kwa mwanafunzi yeyote kuvuta tumbaku aumadawa ya kulevya,kunywa pombe,au kujihusisha na wizi wa aina yoyote.

2.Ni marufuku kwa mwanafunzi kumtembelea mwalimu au mfanyakazi wa shule nyumbani kwake.

3.Ni marufuku mvulana au msichana kuingia katika nyumba au maeneo yaliyojificha.

**C. MAHUDHURIO NA KUWAHI SHULENI**

1.Ni lazima kila mwanafunzi awahi shuleni na kutimiza wajibu kwa kufanya kazi kwa ukamilifu kila siku.

2.Kila mwanafunzi asikose shule.Kama kuna tatizo la ugonjwa taarifa itolewe kesho yake na mzazi au mlezi na sio mwanafunzi mwenzake pamoja na cheti au barua ya daktari aje nayo

shuleni.Ikiwa ni sababu nyingine kama msiba pia taarifa iwasilishwe shuleni kama mwanafunzi amefiwa na ndugu yake,jamaa au mzazi akiwa shuleni taarifa itolewe kwa mkuu wa shule au mwalimu wa darasa .

3.Ruhusa ya kutokuwa shuleni itatolewa tu na mkuu wa shule, makamu wake, mwalimu wa darasa au mwalimu wa zamu.

4.Mwanafunzi haruhusiwi kuondoka katika eneo la shule bila ya ruhusa ya mkuu wa shule au mwalimu
wa zamu.

**MAKOSA YANAYOWEZA KUSABABISHA MWANAFUNZI KUFUKUZWA SHULE.**

i.Wizi
ii.Uasherati
iii.Ulevi na matumizi  ya madawa ya kulevya.
iv.Uvutaji bangi
v.Makosa ya jinai
vii.Kupigana au kupiga
viii.Kuharibu kwa makusudi mali ya umma
ix.Kudharau Bendera ya Taifa
x.Kuoa au kuolewa
xi.Kupata mimba au kusababisha mimba ndani na nje ya shule.
xii.Kutoa mimba
xiii.Kugoma,kuchochea na kuongoza au kuvuruga amani na usalama wa watu.
xiv.Kukataa adhabu kwa makusudi.

**GOVERNMENT OF TANZANIA**
**REQUEST FOR MEDICAL EXAMINATION.**

HEADMISTRESS
VUMARI SECONDARY SCHOOL
P.O.BOX 60
SAME.
DATE …………………

**PART A**:
**TO THE MEDICAL OFFICER**:
………………………………….
………………………………….
………………………………….
**MR/MISS**………………………………………………………………………………
(Name in Full)
Please examination should include the following:

1. a) Eye sight
   b) Hearing
   c) Limbs
   d) Speech
   e) Venereal diseases
   f) Leprosy.
2. Neuroses
3. Other serious diseases

**PART B: MEDICAL CERTIFICATE**:
(To be completed by Government Officer).
I have examined the above named and consider that he/she is physically and Mentally fit/unfit for a full time Secondary School program.

1. a) Eye Sight ………………………………………………………………………
   b) Hearing ………………………………………………………………………
   c) Limbs …………………………………………………………………………
   d) Speech …………………………………………………………………………
   e) Venereal Diseases ……………………………………………………………
   f) Epilepsy ………………………………………………………………………
2. Neurosis ……………………………………………………………………………
3. Other serious diseases …………………………………………………………….

Date ………………………………………...  Signature ……………………………

Station ……………………………………….  Designation ………………………….

**FOMU YA TAARIFA BINAFSI KWA WANAOJIUNGA KIDATO CHA KWANZA VUMARI SEKONDARI**.

1.Jina kamili ………………………………………………………………………………..

2.Jina la mzazi /Mlezi ……………………………………………………………………..

3.Jina la Kata/Kijiji anakotoka mwanafunzi…………………………………………………

4.Jina la Kitongoji ………………………………………………………………………….

5. Je,mwanafunzi anakubaliana na sheria zote za shule ?..........................................

6.Mzazi /Mlezi anakubaliana na taratibu zote za shule?.............................................

7.Je, mwanafunzi anakubali kujifunza na kufikia kiwango kinachokubalika…………………

Uthibitisho.

Jina la mwanafunzi ……………………………Sahihi ……………… Tarehe ………….

Jina la mzazi/ Mlezi ………………………………… Sahihi ……………Tarehe ………….

……………………………………

MKUU WA SHULE

(Fomu hii irudishwe shuleni mtoto anaporipoti)